TANGAZO LA SERIKALI NA. 235 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 811 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6, kwa-

(a) kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikisha kuwa ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (3) na (4) na kuwa kanuni ndogo ya (2) na (3) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 7

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 7 kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (5) kama ifuatavyo:

"(5) Bila kuathiri masharti ya sheria ndogo hii, kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa isiyozidi siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali

hizo.”.

Marekebisho ya kanuni ya 9

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 9 kama ifuatavyo:

Mamlaka ya Afisa Mwidiniwa

9. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri wakati wowote kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.”.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

5. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) kwa kufuta na kuandika upya kipengele cha I cha Sehemu B kama ifuatavyo:

“SEHEMU B

I. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na. | Magari na vifaa vingine | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Isuzu tani 7 | 300,000/= kwa siku |
| 2. | Land cruiser hard top | 200,000/= kwa siku |
| 3. | Land cruiser pick up | 200,000/= kwa siku |
| 4. | Pikipiki | 20,000/= kwa siku |
| 5. | Trekta | 200,000/= kwa tripu |
| 6. | Kukodi boti | 200,000/= kwa safari |
| 7. | Vifaa vya GPS, darubini, spika, Kamera, projector na vifaa vingine vya kielektroniki. | 50,000/= kwa kifaa kwa siku |
| 8. | DGPS RTK | 300,000/= kwa siku |

(b) kwa kufuta na kuandika upya kipengele cha II cha Sehemu G kama ifuatavyo:

“SEHEMU G

II: ADA NA USHURU WA KUENDESHA SHUGHULI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA

| Na. | Aina ya Mchezo | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 2. | Fete | 20,000/= kwa siku |
| 3. | Mashine ya kubetisha au gulugulu | 30,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Ada ya leseni ya mashine ya kubeti | 300,000/= kwa mwaka |

(c) kwa kufuta Kipengele cha 18 cha Sehemu J na kuandika upya kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 18. | Ushuru wa mazao ya mifugo na uvuvi | |
| | (a) Samaki wabichi | 50/= kwa kilo |
| | (b) Samaki wakavu | 50/= kwa kilo |
| | (c) Dagaa wabichi | 20/= kwa kilo |
| | (d) Dagaa wakavu | 40/= kwa kilo |
| | (e) Tenga la kuku | 3,000/= kwa tenga zaidi ya kuku 10 |
| | (f) Samaki wa mapambo | 100/= kwa samaki mmoja” |

(d) katika kipengele cha II cha Sehemu K, kwa kuongeza maneno “kwa kibali” katika nambari 3 hadi nambari 10;
(e) kwa kufuta Sehemu M ya Jedwali la Kwanza;
(f) kwa kubadili mpangilio wa Sehemu N kuwa sehemu M.

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*